JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

KAMATIYA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC)

TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Novemba, 2026

IKISIRI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Uwekezaji wa mitaji ya Umma Mwaka wa Fedha 2024/2025, inawasilishwa Bungeni ili kuliwezesha Bunge kuujadili mwenendo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na kuazimia kuhusu mwenendo huo. Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Kutokana na masharti hayo, Taarifa imegawanyika katika sehemu kuu tatu: Utangulizi, Uchambuzi wa taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na Maoni na Mapendekezo ya Kamati katika Muundo wa hoja uliowekewa masharti kwenye Kanuni ya 64(3) ya Kanuni za Bunge.

Sehemu ya kwanza, inabainisha msingi wa ufuatiliaji wa mitaji ya umma kwa kuzingatia Katiba; Kanuni za Bunge; Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura ya 370; na Sheria nyingine za nchi. Aidha, sehemu hii inabainisha muundo wa uwekezaji wa mitaji ya umma, wigo wa ufuatiliaji wa mitaji ya umma na njia zilizotumika kufuatilia. Njia hizo ni kuchambua taarifa za uwekezaji kwa kuzingatia masharti ya Sheria inayohusika na uwekezaji uliofanyika, kuchambua Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu hali ya jumla ya mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma au kwenye Kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa au kuna maslahi ya umma, na Kufanya mahojiano na Bodi na menejimenti za mashirika au taasisi zinazotumia mitaji ya umma zilizofika mbele ya Kamati.

Sehemu ya Pili, inafafanua hali na mwenendo wa uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa lengo la kubainisha iwapo: Uwekezaji una ufanisi na tija, na kama uwekezaji umezingatia taratibu. Mambo yaliyozingatiwa ni pamoja na michango katika mfuko mkuu wa Serikali. Michango hiyo ni Gawio, Mchango wa 15% ya mapato ghafi, Michango ya 70% ya ziada baada ya gharama za uendeshaji, rejesho la Riba na mikopo na Michango ya TTMS. Jambo lingine muhimu linaloelezwa katika sehemu hii ni ulinganisho wa ufanisi wa mtaji unaowekezwa kwenye taasisi ambapo Serikali ina hisa chache na kule ambapo ina hisa zaidi.

Ufafanuzi katika Sehemu hii, unaonesha kwamba: jumla ya shilingi trilioni 1.028 zilipokelewa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa uchanganuzi ufuatao; Gawio shilingi **Bilioni 612.4**; Mchango wa 15% ya mapato ghafi shilingi **bilioni 333.97;** Ziada na Michango mingineyo shilingi **bilioni 58.8**; Riba na Marejesho ya Mikopo shilingi **bilioni 20.3**; na Michango ya TTMS shilingi **bilioni 3.07**. Vilevile, Sehemu hii ya Pili, inabainisha masuala mbalimbali kuhusu usimamizi na utendaji wa taasisi zinazotumia mtaji wa umma.

Katika sehemu ya Tatu inayohusu maoni na mapendekezo juu ya matokeo ya ufuatiliaji wa Mtaji wa Umma uliowekezwa. Mambo kumi na mbili (12) yamejumuishwa ili kuyajadili na kutolea uamuzi wa Bunge, miongoni mwa hayo ni pamoja na Uwiano mdogo baina ya ongezeko la Uwekezaji ikilinganishwa na rejesho; kuongeza mtaji kwenye hisa chache ili kuongeza faida; kutumia PPP katika miradi yenye fursa hiyo ili kupata fedha na kupunguza

utegemezi; kulipa madeni ya Mamlaka ya Mbolea (TFRA) na kutenga bajeti halisi ya ruzuku ili kuepusha madeni mapya; Tathimini ya kuboresha usimamizi wa rasilimali za NARCO; na tathimini na mabadiliko ya utendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) .

Mwisho, sehemu hii inamalizia kwa kutoa shukurani na pongezi na

mwisho kabisa ni kuhusu hoja kwamba, " Bunge liipokee Taarifa ya Kamati na likubali maoni na mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

YALIYOMO

IKISIRI ..... **i**
YALIYOMO ..... **iv**
ORODHA YA AKRONIMU (ACRONYMS) ..... Error! Bookmark not defined.
ORODHA YA MAJEDWALI ..... **vii**
ORODHA YA GRAFU ..... **viii**
SEHEMU YA KWANZA **1**
1.0 UTANGULIZI **1**
1.1 Maelezo ya Jumla 1
1.2 Muundo wa Taarifa 1
1.3 Msingi wa Shughuli za Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma 2
1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2
1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge 3
1.3.3 Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) Sura ya 370 4
1.3.4 Sheria Mbalimbali kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma 4
1.4 Njia zilizotumika 6
1.5 Muhtasari wa Sehemu ya Kwanza 7
SEHEMU YA PILI **9**
2.0 UFAFANUZI WA SHUGHULI ZA KAMATI KUFUATILIA MITAJI YA UMMA **9**
2.1 Maelezo ya Jumla 9
2.2 Hali ya Jumla ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma 10
2.3 Tathmini ya Ufanisi wa Mitaji ya Umma katika Kampuni ambako Serikali ina hisa chache 12
2.3.1 Mwenendo wa Thamani ya Hisa kwenye Vitegauchumi ambako Serikali ina hisa chache 14
2.3.2 Gawio (Dividend) kutoka kwenye Vitegauchumi ambako Serikali ina Hisa Chache 17
2.4 Tathmini ya Ufanisi wa Mitaji katika Vitegauchumi vya Umma 18
2.5 Mambo ya Jumla kuhusu Uendeshaji wa Mitaji ya Umma 29
2.5.1 Umuhimu wa Kufungamanisha Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi na Dira ya Taifa ya 2050 29
2.5.2 Mpango wa Kushirikisha Sekta binafsi (PPP) katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa na taasisi/mashirika ya umma 31
2.5.3 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini katika Mishahara na uendeshaji 33
2.5.4 Tathimini ya Utendaji wa taasisi na Mashirika ya umma 35
2.5.5 Mapungufu katika Utendaji wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko 40

2.5.6 Athari ya Deni la Tozo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Kampuni ya STAMIGOLD 42
2.5.7 Changamoto ya Madeni kwa Mamlaka ya Mbolea (TFRA) 43
2.5.8 Mwenendo wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*) 45
2.5.9 Athari ya Mtaji katika Kampuni ya Ranchi za Taifa (*NARCO*) 46
2.5.10 Uzingatiaji wa Vigezo vya Utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina 49
SEHEMU YA TATU 53
3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO 53
3.1 Maoni Kutokana na Uchambuzi 53
3.1.1 Ongezeko la Mtaji wa Umma 53
3.1.2 Uwekezaji katika Taasisi Ambazo Serikali Inamiliki Hisa Chini ya Asilimia 50 53
3.1.3 Michango ya Mashirika ya Umma katika Mfuko Mkuu wa Serikali 54
3.1.4 Utegemezi wa Ruzuku ya Serikali 54
3.1.5 Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma 54
3.1.6 Ushirikiano na Sekta Binafsi katika Miradi ya Maendeleo 54
3.1.7 Madeni ya Ruzuku ya Mbolea kwa TFRA 54
3.1.8 Deni la VAT la STAMIGOLD 55
3.1.9 Mipango ya Taasisi na Dira ya Taifa ya 2050 55
3.1.10 Utendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) 55
3.1.11 Usimamizi wa Rasilimali za NARCO 55
3.1.12 Uzingatiaji wa Vigezo vya Utendaji 55
3.2 Mapendekezo 56
3.2.1 Ongezeko la Mtaji wa umma katika taasisi na Mashirika ya Umma 56
3.2.2 Ongezeko la Thamani ya Uwekezaji katika taasisi ambapo Mtaji wa umma ni pungufu ya asilimia 50 57
3.2.3 Mchango wa Mashirika ya Umma katika Mfuko Mkuu wa Serikali 58
3.2.4 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini 59
3.2.5 Tathmini ya Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma 60
3.2.6 Mpango wa Kushirikisha Sekta Binafsi katika Miradi ya Maendeleo ya Taasisi na Mashirika ya Umma 61
3.2.7 Changamoto ya Madeni ya Ruzuku ya Mbolea kwa Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) 61

3.2.8 Athari za Deni la Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Kampuni ya STAMIGOLD 62
3.2.9 Umuhimu wa Kufungamanisha Mipango ya Taasisi na Dira ya Taifa ya 2050 63
3.2.10 Mwenendo wa Utendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) 64
3.2.11 Athari za Upungufu wa Usimamizi wa Rasilimali katika Tija ya Mtaji wa Umma wa NARCO 65
3.2.12 Uzingatiaji wa Vigezo vya Utendaji katika Usimamizi wa Mtaji wa Umma 66
SEHEMU YA NNE..... 67
4.0 **HITIMISHO**.....67
4.1 Shukurani.....67
4.2 Hoja 69
VIAMBATISHO.....71
KIAMBATISHO NA 1: TAASISI NA MASHIRIKA YALIYOKUTANA NA KAMATI YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI, 2026 HADI NOVEMBA, 2026 71
KIAMBATISHO 02: ORODHA YA UWEKEZAJI WA SERIKALI KWENYE TAASISI AMBAPO SERIKALI INA *HISA CHACHE (MIS)* 101

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Jedwali la Hali ya Umiliki wa Hisa Chache za Serikali kwa Mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025 13

Jedwali Na. 2: Mwenendo wa Mapato yasiyo ya Kikodi kwa Kipindi cha Mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025 19

ORODHA YA GRAFU

Grafu Na. 1: Mwenendo wa Thamani ya Hisa za Serikali katika Vitega Uchumi ambapo Serikali ina hisa chache 15

Grafu Na. 2: Mwenendo wa Makusanyo ya Gawio Mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025.....17

Grafu Na. 3: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Gawio kutoka Taasisi ambazo Serikali ina Hisi Nyingi.....20

Grafu Na. 4: Mwenendo wa Makusanyo ya Machango wa asilimia n15 ya Mapato Ghafi 22

Grafu Na. 5: Mwenendo wa Makusanyo ya Michango ya Asilimia 70 ya ziada ya Mapato.....24

Grafu Na. 6: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Riba kwa mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025.....25

Grafu Na. 7: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato kutokana na TTMS kwa kipindi cha 2022/2023 hadi 2024/2025 27

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 139(16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Uwekezaji wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, na kuliomba Bunge likubali kuipokea na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inalenga kuliarifu Bunge lako Tukufu juu ya Mwenendo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Serikali kwa lengo la kutoa maazimio ikiwa ni sehemu ya Bunge kutekeleza jukumu lake la kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuleta ustawi wa jamii.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mhesimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza inahusu mambo ya jumla ambayo ni Utangulizi.

(ii) Sehemu ya pili inatoa ufafanuzi wa shughuli za Kamati kuhusu ufuatiliaji wa mitaji ya umma katika taasisi na mashirika ya umma pamoja na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

(iii) Sehemu ya tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya ili Bunge likiridhia yawe maazimio ya Bunge kwa mambo yaliyojitikeza katika uwekezaji wa mitaji ya umma.

(iv) Sehemu ya Nne inahitimisha taarifa hii kwa kuliomba Bunge liipokee taarifa na kuijadili.

1.3 Msingi wa Shughuli za Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, Msingi wa shughuli za Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni kuhakikisha kwamba Serikali, kwa niaba ya wananchi, inapata thamani inayostahili kutokana na mitaji ya umma iliyowekezwa. Msingi huu ni katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge yaliyofafanuliwa katika Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (Katiba) kuwa Bunge lina Madaraka ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote kwa namna iliyowekewa masharti kwenye Kanuni za Bunge. Pamoja na masharti hayo, Kamati huzingatia sheria mbalimbali wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Kwa ufafanuzi zaidi misingi ya shughuli za Kamati ni kama ifuatavyo:-

1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Serikali inamiliki au inawekeza mitaji katika mashirika na kampuni mbalimbali, Bunge lina msingi wa kikatiba wa kufuatilia namna mali na mitaji hiyo ya umma inavyosimamiwa. Kwa muktadha huu, Katiba imekuwa msingi wa shughuli za Kamati hii kwa kuonesha

madaraka ya Bunge na kuruhusu kutungwa kwa Kanuni za Bunge zinazoweka utaratibu wa utekelezaji wa madaraka ya Bunge katika kusimamia uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Kwa vyovyote vile Kamati haikupaswa kutoka nje ya msingi huu na kwa kweli masharti yote yalizingatiwa.

1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Bunge zinatoa mwongozo kuhusu utaratibu, desturi na uendeshaji wa shughuli zote zinazohusu utekelezaji wa madaraka ya Bunge. Kanuni za Bunge zimeundwa kwa kuzingatia Ibara ya 89 ya Katiba ya Tanzania, aidha, Ibara ya 96 (1) imetoa fursa ya kuanzisha Kamati za Kudumu za Bunge, ambapo kwa kutumia fursa hiyo Kamati mbalimbali za bunge ikiwemo Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma zimeundwa kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 140 ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kanuni zinafafanua utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zote za Kamati za Bunge, ambapo kwa mujibu wa kanuni hizi Kamati PIC ndio Jicho la Bunge katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, jukumu hili limefafanuliwa katika Kifungu cha 11 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Jukumu hilo linahusu uchambuzi na ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma uliowekezwa kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa nyingi na kule ambapo Serikali ina hisa chache kwa lengo la kuhakikisha

kuna utekelezaji wenye tija, ufanisi na unaoleta thamani halisi ya mtaji uliowekezwa.

1.3.3 Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) Sura ya 370

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura ya 370, imeanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina (OMH). Madhumuni ya Kuanzishwa kwake ni utwaaji (*acquisition*), umilikaji (*holding*) na usimamizi (*management*) wa mitaji ya umma kwa niaba ya Serikali. Kwa mujibu wa Sheria hii, mitaji ya umma ni pamoja na hisa (shares), hati fungani (government bonds), dhamana ya hisa ya mikopo, rehani ya ndani au nje ya bodi inayotambulika kisheria, ambayo imetolewa na Serikali au kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, majukumu na madaraka ya Msajili wa Hazina (TR) katika uwekezaji wa mitaji ya umma unaofuatiliwa na Kamati yamebainishwa katika Sheria hii. Kwa msingi huo, Kamati ilipofuatilia mitaji ya umma ilitathmini uendeshaji wa mitaji ya umma ili kubaini iwapo kuna ukubalifu (*Compliance*) wa masharti ya Sheria hii kuhusu usimamizi wa mitaji ya umma.

1.3.4 Sheria Mbalimbali kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, pamoja na Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), sheria nyingine zinazofafanua masharti kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma zilizingatiwa wakati wa kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma. Sheria

hizo kutaja baadhi, ni Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 na Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mashirika ya Umma imeweka masharti kuhusu uanzishaji, usimamizi, uongezaji wa ufanisi na mambo mengine ambayo yanahusiana au yanayowezesha madhumuni hayo. Kwa msingi huo, Kamati, ilizingatia masharti ya Sheria hii na kutathmini iwapo uwekezaji na usimamizi wa mitaji katika mashirika ya umma unafanyika kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Umma, imeweka masharti ya udhibiti, usimamizi na udhubiti wa makusanyo na matumizi ya fedha za umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, sheria hii imebainisha masharti ya udhibiti na usimamizi wa kibunge wa fedha na rasilimali za umma. Vilevile sheria inatambua kwamba, fedha zinazotumika katika mtaji wa umma, mali zilizopo katika vitega uchumi vitokanavyo na fedha za umma na mikopo katika uendeshaji wa vitega uchumi ni sehemu ya rasilimali za umma. Kamatiilitathmini chumo (*returns*) kutokana na fedha za umma linapaswa kuangaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, inampa Msajili wa Hazina Madaraka na Majukumu ya kusimamia fedha zinazotolewa kwa ajili ya uwekezaji kwenye taasisi au mashirika anayoyasimamia. Kwa mujibu wa sheria hiyo,

Msajili wa Hazina analo jukumu na madaraka ya kuhakikisha kwamba mashirika na taasisi ambazo anazisimamia zinalipa magawio na michango stahiki kwa Serikali. Kamati ilifuatilia kujua utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Msajili ya kusimamia fedha zinazotumika katika mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla miongozo yote hii, Katiba ya JMT, Kanuni za Kudumu za Bunge, Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sheria ya Fedha za Umma, Sheria ya Mashirika ya Umma, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 vimezingatiwa na Kamati katika kufanya uchambuzi wa taarifa zilizofika mbele yake.

1.4 Njia zilizotumika

Mheshimiwa Spika, naomba kubainisha mbinu zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamatikwa kipindi kinachoripotiwa. Mbinu hizo ni:

(i) Kuchambua masharti ya Sheria inayohusika na uwekezaji uliofanyika katika taasisi/shirika husika kwa lengo la kubaini uhalali wa uanzishwaji wake na uendeshaji uliotakiwa;

(ii) Kupokea na kuchambua Taarifa za Msajili wa Hazina (TR) kuhusu hali ya jumla ya mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma au kwenye Kampuni ambapo Serikali ina umiliki wa hisa au kuna maslahi ya umma kwa lengo la ufanisi wake;

(iii) Kufanya mahojiano na menejimenti na Bodi za taasisi au mashirika ambayo yanatumia mitaji ya umma.

Lengo ni kuthibitisha usahihi wa hali ya mitaji ya umma kwenye taasisi husika kabla ya kutoa taarifa Bungeni; na

(iv) Kutembelea na kukagua hali ilivyo kwenye baadhi ya miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na taasisi na mashirika ambayo yanatumia mitaji ya umma.

1.5 Muhtasari wa Sehemu ya Kwanza

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya kwanza imetoa utangulizi wa Taarifa hii kwa kubainisha muundo wa taarifa na msingi wa kikatiba na kisheria ulioongoza shughuli za Kamati. Aidha, imebainisha mbinu nne zilizotumika katika ufuatiliaji na tathmini ya hali ya uwekezaji pamoja na ufanisi wa mitaji ya umma. Mambo makuu matano yanayojitokeza ni:

(i) Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977, imelipa Bunge madaraka ya kusimamia na kuishauri Serikali. Madaraka hayo yanapaswa kuzingatia lengo kuu la Serikali la ustawi wa wananchi;

(ii) Bunge linaitumia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya umma kama jicho lake katika uwekezaji wa mitaji ya umma. Hii inatokana na msingi uliowekwa na Kanuni ya 140 na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kuhusu Muundo na majukumu ya Kamati za Bunge;

(iii) Ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma na ufanisi wa hali ya mitaji hiyo unafanyika kwa misingi ya kisheria. Sheria zinazohusika moja kwa moja ni: Sheria

ya Msajili wa Hazina (Sura ya 370), Sheria ya Mashirika ya Umma (Sura ya 257), Sheria ya Bajeti (Sura ya 439) na Sheria ya Fedha za Umma (Sura ya 348);

(iv) Taarifa hii ni matokeo ya kazi ya Kamati iliyofanyika kwa kutumia mbinu zinazojumuisha kuchambua sheria, kupokea taarifa za Msajili wa Hazina, kufanya mahojiano na Bodi kwa pampja na menejimenti za taasisi zinazotumia mtaji wa umma na kutembelea miradi ya uwekezaji; na

(v) Taarifa hii inalenga kuliarifu Bunge kuhusu hali na ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma, ili kuwezesha kutoa maazimio katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mambo hayo yanatoa mwelekeo wa jumla wa Taarifa hii. Lengo lake ni kubainisha maeneo yanyohitaji umakini, kuepusha mkanganyiko na kurahisisha misingi ya uamuzi wa kupitisha maazimio ya Bunge.

SEHEMU YA PILI

2.0 UFAFANUZI WA SHUGHULI ZA KAMATI KUFUATILIA MITAJI YA UMMA

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya pili ya taarifa hii inafafanua shughuli za Kamati za kufuatilia mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma na kwenye vitega uchumi ambapo kuna hisa za Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, lengo likiwa ni kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufanya uamuzi kuhusu matokeo ya ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma.

Ili kufanikisha azma hiyo, sehemu hii imegawanyika katika sehemu ndogo mbili: Sehemu ndogo ya kwanza inatoa maelezo kuhusu hali ya mtaji wa umma uliowekezwa hadi kufikia 2024/2025 na sehemu ndogo ya pili inahusu mambo mbalimbali yaliyobainika kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo niliioueleza, sehemu hii inaripoti shughuli zilizofanywa na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ya kufuatilia mwenendo na masuala mengine ya mitaji ya umma kwa lengo la kutoa taarifa na mapendekezo yatakayoliwezesha Bunge kuchukua nafasi yake ya usimamizi na kuamua kulingana na madaraka yake.

2.2 Hali ya Jumla ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji wa mitaji ya umma ni mchakato ambapo Serikali kwa kutumia rasilimali za umma, inaweka fedha, mali au mitaji katika taasisi, mashirika ya umma au kampuni kwa lengo la kupata manufaa ya kiuchumi, kijamii au kimkakati kwa Taifa. Uwekezaji huu unaweza kufanywa kupitia ununuzi wa hisa katika kampuni, kuingiza mtaji katika mashirika ya umma, kugharamia miradi ya kimkakati au kushiriki katika uwekezaji wa pamoja. Mitaji hiyo inapaswa kusimamiwa kwa uwazi, uwajibikaji na ufanisi kwa kuwa inatokana na rasilimali zinazomilikiwa na umma.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mtaji wa umma uliowekezwa katika taasisi, mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali inaumiiki wa hisa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imefikia shilingi trilioni 92.275. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa uwekezaji huu umeendelea kukua ambapo kwa miaka mitatu mfululizo umeongezeka kutoka Shilingi trilioni 76.708 mwaka 2022/23 hadi Shilingi trilioni 92.275 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la takribani asilimia 20.3.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa mtaji wa ummma ambao umekwishwa wekezwa na Serikali hadi kufikia mwaka 2024/2025 unaweza kugawanywa katika makundi yafuatayo:-

Uwekezaji kwa umiliki wa Hisa

(i) Uwekezaji katika taasisi, mashirika ambayo inaumilikiwa asilimia 51 au zaidi ni takribani shilingi bilioni 89.01 kiasi

hiki ni ongezeko la asilimia 6 ukilinganisha na shilingi 83.97 kwa mwaka 2023/2024.

(ii) Uwekezaji katika taasisi ambazo inaumiliki wa hisa pungufu ya asilimia 50 ni takribani shilingi **3.267** hili ni ongezeko la asilimia 52.2 ukilinganisha na shilingi **2.147** kwa mwaka 2023/2024.

Uwekezaji kwa Eneo la Kijigrafia (Geografical Location)

(i) Uwekezaji katika taasisi za ndani ya nchi ni takribani shilingi trilioni 90.6, hapa kunaongezeko la asilimia 6.1 ukilinganisha na shilingi 85.38 zilizokuwa mwaka 2023/24.

(ii) Uwekeza katika taasisi zilizopo nje ya nchi ni takribani shilingi trilioni 1.675, sawa na ongezeko la asilimia 98 ukilinganisha na shilingi bilioni 846.22 kwa mwaka 2023/24;

Uwekezaji kwa aina ya majukumu/shughuli (ya Biashara na yanayotoa huduma)

(i) Uwekezaji katika taasisi za zinazojiendesha kibiashara ni takribani shilingi trilioni 25.168, hapa kunaongezeko la asilimia 1.5 ukilinganisha na shilingi trilioni 24.79 zilizokuwa mwaka 2023/24.

(ii) Uwekeza katika taasisi zinazotoa huduma ni takribani shilingi 65.441, sawa na ongezeko la asilimia 8 ukilinganisha na shilingi 60.59 kwa mwaka 2023/24.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kategoria zote za uwekezaji tumeshuhudia Serikali ikiendelea kuongeza kiasi cha mtaji wa umma kilichowekeza kwenye taasisi na mashirika ya umma. Kamati inatoa rai kwa Bodi za wakarugenzi za taasisi na mashirika ya umma kutambua kwamba Kadiri uwekezaji huu unavyoongezeka, ndivyo wajibu wa kuulinda, kuuendeleza na kuhakikisha unazalisha tija kwa Taifa na wananchi unavyoongezeka. Ni vyema wakaongeza jitihada na mikakati itakayolinda uwekezaji huu ili tija stahiki iweze kupatikana.

2.3 Tathmini ya Ufanisi wa Mitaji ya Umma katika Kampuni ambako Serikali ina hisa chache

Mheshimiwa Spika, Hisa za Serikali kama sehemu ya mtaji wa umma zinaweza kuwa katika vitegauchumi ambapo Serikali ina hisa chache au katika vitegauchumi ambapo Serikali ina hisa nyingi. Msajili wa hazina amewa jukumu la kufuatilia uwekezaji huo unaohusisha natumnizi ya rasilimali za umma. Kwa kuwa tija ya mtaji wa umma katika uwekezaji huo inahtajika, Kamati ilifanya ufuatiliaji na kuchambua mwenendo wa hisa hizo kwa miaka mitatu mfululizo. Hali ya uwekezaji huo inaonekana katika **Jedwali Na. 1**.

Jedwali Na. 1: Jedwali la Hali ya Umiliki wa Hisa Chache za Serikali kwa Mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025

MWAKA	IDADI YA TAASISI ZENYE HISA CHACHE	(TRILIONI) THAMANI YA HISA CHACHE	IDADI YA TAASISI AU KAMPUNI ZILIZOTOA GAWIO	KIASI CHA GAWIO	ASILIMIA
2022/2023	56	2.147	15	281.22	13
2023/2024	56	2.76	17	195.43	7
2024/2025	56	3.267	18	293.41	8.9

Chanzo: *Majumuisho ya Taarifa za Msajili wa Hazina*

Mheshimwa Spika, jedwali hilo linaonesha kuwa:

(i) Thamani ya hisa imeongezeka kwa kasi kwa miaka mitatu mfululizo, lakini kasi ya ukuaji imepungua kutoka 28.5% hadi 18.4%. Hii inaonyesha uwekezaji bado unakua, lakini si kwa kasi ile ile.

(ii) Idadi ya taasisi kwa miaka yote mitatu imebaki 56. Hii inaonesha hakuna mabadiliko kwenye muundo wa umiliki wa Serikali katika kundi hili. Serikali haijaongeza wala kupunguza taasisi zenye hisa chache.

(iii) Idadi ya taasisi zinazotoa gawio imeongezeka kidogo kutoka 15 hadi 18 kati ya 56. Hii inaonyesha uboreshaji mdogo wa uwajibikaji, lakini bado asilimia 67.9 ya taasisi hizo hazikutoa gawio mwaka 2024/25, hali inayohitaji ufuatiliaji wa karibu.

(iv) Uwiano wa gawio kwa thamani ya hisa umeshuka kutoka asilimia 13 mwaka 2022/23 hadi asilimia 8.9

mwaka 2024/25. Hii inaonesha kwamba, ingawa thamani ya hisa inaongezeka, gawio haliongezeki kwa kiwango sawa. Mwenendo huo ni ishara ya kupungua kwa ufanisi wa hisa kuzalisha gawio.


Mheshimiwa Spika, kwa ujumla thamani ya hisa imeongezeka kwa **asilimia 52.2** kwa miaka mitatu, lakini idadi ya taasisi zinazotoa gawio ni 18 kati ya 56 sawa na **asilimia 32.1.** Aidha, uwiano wa gawio kwa thamani ya hisa umeshuka kutoka **asilimia 13** hadi **asilimia 8.9**.

2.3.1 Mwenendo wa Thamani ya Hisa kwenye Vitegauchumi ambako Serikali ina hisa chache

Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu linapofuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma, linahitaji kujua tija ya uwekezaji kwa kipimo cha mwenendo wa hisa za serikali pamoja na viashiria vingine. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Kamati ilichambua mwenendo wa uwekezaji kuanzia mwaka 2022/2023 hadi mwaka 2024/2025. **Grafu Na. 1** inabainisha mwenendo huo.

Grafu 1 Thamani ya Hisa za Serikali kwa Miaka mitatu

Grafu Na. 1 Mwenendo wa Thamani ya Hisa za Serikali katika Vitega Uchumi ambapo Serikali ina hisa chache



Chanzo: Majumuisho ya Vikao vya Kamati kwa ajili ya Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, mwenendo huo unaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Thamani ya uwekezaji wa Serikali kwenye kampuni au taasisi ambapo ina hisa chache, imeendelea kuongezeka kwa miaka mitatu mfululizo kutoka **shilingi trilioni 2.147** mwaka 2022/2023 na kufikia **shilingi trilioni 2.76** mwaka 2023/2024. Ogezeko hilo la thamani lilifikia **shilingi trilioni 3.267** mwaka 2024/2025.

(ii) Ongezeko la thamani ya hisa haikufanana kwa vipindi tofauti. Kati ya mwaka 2022/2023 na 2023/2024 thamani ya hisa iliongezeka kwa **28.5%** na kati ya mwaka 2023/2024 na 2024/2025, hisa iliongezeka kwa **18.4%**

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huo unalijulisha Bunge mambo yafuatayo:-

(i) Uwekezaji wa Serikali katika kampuni au taasisi ambapo ina hisa chache umekuwa na ukuaji chanya na endelevu kwa miaka mitatu mfululizo, jambo linaloashiria kwamba mtaji wa umma unaongezeka thamani kwa muda. Hali hii ni dalili ya tija ya uwekezaji na inaonesha kuwa Serikali inafanya uamuzi sahihi wa kuwekeza katika sekta zinazohusika.


(ii) Pamoja na mwenendo wa uwekezaji kuonesha ishara ya uwekezaji wenye tija, kasi ya ukuaji wa hisa imepungua kutoka asilimia 28.5 (2022/2023 –2023/2024) hadi asilimia 18.4 (2023/2024 –2024/2025). Kupungua huku ni ishara ya tahadhari kwamba uwekezaji unaweza kukumbwa na changamoto zinazopunguza kasi ya ukuaji.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa thamani ya hisa pekee haiwezi kutoa picha kamili ya tija, viashiria vingine muhimu vinapaswa kuoanisha mwenendo huu. Mathalani gawio, chumo (ROI), ubora wa usimamizi, mchango kwa uchumi, ulinganisho na soko na uendelevu. Viashiria vyote kwa pamoja vinawezesha kubaini kama ongezeko la thamani linaakisi tija halisi au ni athari ya mazingira ya soko pekee.

2.3.2 Gawio (Dividend) kutoka kwenye Vitegauchumi ambako Serikali ina Hisa Chache

Mheshimiwa Spika, kuchambua mwenendo wa gawio kutoka vitegauchumi ambako Serikali ina hisa chache ni muhimu. Kwa kawaida gawio ni ushahidi wa moja kwa moja wa faida halisi, tofauti na thamani ya hisa inayoweza kupanda kwa uvumi au mfumuko wa bei. Mwenendo huu hupima tija ya uwekezaji kwa fedha halisi, hubaini ubora wa usimamizi na hulinda maslahi ya wananchi kwa kuhakikisha mali ya umma inazaa faida. Kwa muktadha huo, mwenendo wa gawio kwa miaka mitatu inayotumika katika uchambuzi unaonekana katika **Grafu Na. 2**.

Grafu Na. 2: Mwenendo wa Makusanyo ya Gawio Mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025



Mheshimiwa Spika, mwenendo wa gawio kwa miaka mitatu unaonesha kwamba, kiasi cha gawio kilianza kwa Shilingi bilioni 281.22 mwaka 2022/2023, kikashuka hadi Shilingi bilioni 195.43 mwaka 2023/2024, na kisha kupanda hadi Shilingi

bilioni 293.41 mwaka 2024/2025. Uchambuzi wa mwenendo huu unaonesha yafuatayo:

(i) Mwenendo wa gawio haukuwa thabiti na kwamba gawio lilipungua kwa asilimia 30.5 kati ya mwaka wa kwanza na wa pili, kisha likapanda kwa asilimia 50.1 kati ya mwaka wa pili na wa tatu.

(ii) Kupungua kwa gawio mwaka 2023/2024 ni ishara ya tahadhari kwamba baadhi ya kampuni zinaweza kuwa zilikumbwa na changamoto za usimamizi, mazingira magumu ya biashara, au madeni yaliyopunguza faida inayogawanywa.

Mheshimiwa Spika, hali hii inadhihirisha kwamba ongezeko la thamani ya hisa halikuakisiwa moja kwa moja katika gawio halisi kwa mwaka huo. Hata hivyo, kupanda kwa gawio mwaka 2024/2025 hadi kufikia kiwango cha juu kuliko mwaka wa kwanza ni dalili ya ahueni na uwezekano wa kuboreshwa kwa usimamizi na mikakati ya kampuni zinazohusika.

2.4 Tathmini ya Ufanisi wa Mitaji katika Vitegauchumi vya Umma

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa vitegauchumi ambavyo Serikali ina hisa chache, Bunge linao wajibu wa kusimamia ufanisi wa mitaji ya umma katika taasisi na mashirika ya umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ilifuatilia hali ya mitaji ili kujiridhisha kuhusu uwazi, uwajibikaji na uamuzi unaolinda maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetathmini ufanisi wa Serikali katika kukusanya mapato yasiyokuwa ya kikodi kutokana na uwekezaji wa mitaji kwenye vitegauchumi vya umma. Mapato hayo ni gawio, Mchango (15%), Ziada & Michango Mengineyo, Riba na Marejesho ya Mikopo, Wasilisho la mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa katika Mfumo wa Ufuatiliaji wa Trafiki ya Mawasiliano. Hali na mwenendo wa mapato hayo kwa miaka mitatu unaonekana katika **Jedwali Na. 2.**

Jedwali Na. 2: Mwenendo wa Mapato yasiyo ya Kikodi kwa Kipindi cha Mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025

Mapato yasiyo ya kikodi	Kiasi Kilichopokewa			Tofauti katika %
	2022/2023	2023/2024	2024/ 2025	
Gawio	328,746,772,163.7	309,863.304,720.3	612,408,290,180.	86.2
Mchango (15%)	346,280,991,227.6	324,573,038,459.2	333,975,788,606.	(3.5)
Ziada & Michango Mengineyo	287,212,061,547.5	67,724,238,270.0	58,830,969,326.	(79.5)
Riba na Marejesho ya Mikopo	36,039,502,125.0	58,980,610,653.8	20,293,173,068	(43.6)
Wasilisho la TTMS	10,109,407,646.5	5,943,530,559.4	3,077,443,623	(7)
JUMLA	1,008,388,734,710.3	767,084,722,662.6	1,028,585,664,803	2

Chanzo: *Majumuisho ya Kamati kutokana na Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Msajili wa Hazina*


Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba, chumo la uwekezaji (Return on Investment) kwa mwaka 2024/25 limeongezeka kwa asilimia 25.4 ikilinganishwa na mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo limechangiwa kwa kiasi kikubwa na uchangiaji unaotokana

na gawio ambalo limeongezeka kwa aslimia 97.6. Uchambuzi wa kila aina ya mapato ulifanyika kwa lengo la kupata hali halisi ya ufanisi na sehemu zinazohitaji ushauri mahsusi wa kibunge.

(a) Uchambuzi wa Gawio

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kampuni, Sura ya 180 pamoja na Kifungu 15 (2) (b) cha Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 imeweka masharti yanayowezesha Serikali kupata gawio. Kwa kawaida, gawio ni kipimo cha faida halisi inayopatikana kutokana na mtaji wa umma. Hivyo mwenendo wa gawio unatumika kuonesha manufaa yanayotokana na uwekezaji wa mitaji ya umma. Uchambuzi wa mwenendo huo unaonekana katika **Grafu Na. 3**.

Grafu Na. 3 Mwenendo wa Ukusanyaji wa Gawio kutoka Taasisi ambazo Serikali ina Hisi Nyingi



Chanzo: *Majumuisho yaliyofanywa na Kamati kuhusu Mwenendo wa Upokeaji wa Gawio kwa miaka mitatu*.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huo unaonesha yafuatayo:

(i) Mwaka 2022/2023, Serikali ilipokea gawio la **TSh. bilioni 328.75** na likapungua hadi TSh. bilioni 309.86 mwaka 2023/2024, sawa na kupungua kwa takribani **asilimia 5.7** ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.

(ii) Mwaka 2024/2025, gawio liliongezeka hadi **TSh bilioni 612.41** sawa na ongezeko la takribani **asilimia 97.6** ikilinganishwa na mwaka 2023/2024.

(iii) Kwa ujumla, gawio liliongezeka kwa takribani **asilimia 86.2** kati ya mwaka 2022/2023 na 2024/2025, jambo linaloonesha ongezeko la mapato ya Serikali kutokana na uwekezaji wa mitaji ya umma.


(b) Mchango (15%) ya Mapato Ghafi kwa Mwaka

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 9(1)(f) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura ya 370, kinampa Msajili wa Hazina mamlaka ya kuyataka mashirika yasiyofanya biashara kutoa **asilimia 15** ya mapato ghafi (*Gross Revenue*) kwa mwaka na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali (*Consolidated Fund*). Vilevile, Kifungu cha 12 (3) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 kinataka wakala wa Serikali au shirika la umma ambalo linatoza na kukusanya ada kwa hudumu iliyotoa, kuchangia **asilimia 15** ya mapato ghafi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, uchambuzi wa mwenendo wa mapato ghafi kwenye mfuko mkuu wa Serikali, unaliwezesha Bunge kubaini iwapo kuna uzingatiaji

wa sheria katika uwekezaji wa mitaji ya umma. Kwa muktadha huo, mwenendo wa upatikanaji wa michango hiyo unaonekana katika **Grafu Na. 4.**

Grafu Na. 4: Mwenendo wa Makusanyo ya Machango wa asilimia n15 ya Mapato Ghafi



Chanzo: *Tathmini ya Uzingatiaji wa Sheria ya Msajili wa Hazina inayoelekeza kiasi cha Michango ya Mapato Ghafi.*

Mheshimiwa Spika, mwenendo huo unabainisha yafuatayo:

(i) Michango ya **asilimia 15** ya mapato ghafi (*Gross Revenue*) kwa mwaka ilipungua kutoka **TSh bilioni 346.28** mwaka 2022/2023 hadi **TSh bilioni 324.57** mwaka 2023/2024 ikiwa ni upungufu wa **asilimia 6.3**.

(ii) Mwaka 2024/2025 michango ilirejea kuongezeka kwa kiasi kidogo hadi **TSh bilioni 333.98** ikiwa ni ongezeko la takribani **asilimia 2.9**.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huo kwa ujumla, unaonesha utulivu katika kipindi cha miaka mitatu, ukisalia katika kiwango cha kati ya **TSh bilioni 325** na **Tsh. Bilioni 346**.


Kiwango hicho kilipungua kwa jumla kwa **asilimia 3.5** kwa kuzingatia mwaka wa kwanza wa ukokotozi (*base year*) na mwaka wa kufanyia kazi (*current year*). Hali hiyo inaashiria kiwango cha uthabiti wa chanzo hiki cha mfuko mkuu wa Serikali inagwa kuna haja ya kuongeza usimamizi kwa taasisi au mashirika yasiyochangia ipasavyo.

(c) Mchango wa Asilimia 70 ya Ziada baada ya Gharama za Uendeshaji

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12(2) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura ya 370, kimeweka masharti kwamba, taasisi inayotumia mtaji wa umma katika uwekezaji itapaswa kuchangia kwenye mfuko mkuu wa serilai, asilimia 70 ya ziada ya mapato yake baada ya gharama za uendeshaji. Uchambuzi wa mchango huu, unatoa picha kamili ya utekelezaji wake, unabaini kama mashirika yanawasilisha kiasi stahiki cha salio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na unawezesha Bunge kupima ufanisi wa usimamizi wa Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa ukusanyaji wa michango hiyo iliyowekwa kwa mujibu wa sheria unaonekana katika **Grafu Na. 5.**

Grafu Na. 5: Mwenendo wa Makusanyo ya Michango ya Asilimia 70 ya ziada ya Mapato



Chanzo: *Tathmini ya Uzingatiaji wa Sheria ya Msajili wa Hazina inayoelekeza kiasi cha Michango ya 70% ya ziada.*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa mwenendo huo unabainisha yafuatayo:-

(i) Makusanyo ya asilimia 70 ziada ya mapato baada kuondoa gharama za uendeshaji yalishuka kwa kasi kubwa sana kutoka **TSh bilioni 287.21** mwaka 2022/2023 hadi **TSh bilioni 67.72** mwaka 2023/2024, sawa na kupungua kwa asilimia **76.4%.**

(ii) Makusanyo yaliendela kushuka kwa kiasi kidogo mwaka 2024/2025 hadi kufikia **TSh bilioni 58.83**, sawa na kupungua kwa ziada kiwango cha asilimia **13.1%** ikilinganishwa na mwaka 2023/2024.

(iii) Kwa ujumla, katika kipindi cha miaka mitatu, mchango huu umepungua kwa asilimia 79.5.

Mheshimiwa Sika, kwa ujumla mwenendo huo, unaashiria kuna haja ya kuongeza jitihada katika kusimamia gharama ya uendeshaji za taasisi na mashirika ya umma kwa lengo la


kuyadhibiti na kuendelea kupata tija iliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

(d) Makusanyo ya Riba na Marejesho ya Mikopo

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11(2)(o) cha Sheria ya cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura ya 370 kimempa Msajili wa Hazina Jukumu la kufuatilia Ruzuku za mitaji (*Capital grants*), Ruzuku ya kusaidia uendeshaji (*Subsidy*), fedha za mtaji kwa uwekezaji wa muda mrefu (*Capital funds*) na akiba (Reserves). Kwa msingi huo, Kamati ilichambua mwenendo wa makusanyo ya Riba na Marejesho ya Mikopo ili kubaini uwezekano wa hasara na kuliwezesha Bunge kutoa maazimio ya kimfumo ya kuimarisha ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa makusanyo hayo kwa miaka mitatu unaonekana katika **Grafu Na. 6.**

Grafu Na. 6: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Riba kwa mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025



Chanzo: *Tathmini ya Ukusanyaji wa Riba na Marejesho ya Mikopo kwa kipindi cha 2022/2023 – 2024/2025*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha yafuatayo:-

(i) Riba na marejesho ya mikopo yaliongezeka kutoka **TSh bilioni 36.04** mwaka 2022/2023 hadi **TSh bilioni 58.98** mwaka 2023/2024 ikiwa ni ongezeko la la **asilimia 63.6**;

(ii) Mwaka 2024/2025 yalipungua kwa kiasi kikubwa hadi **TSh bilioni 20.29**, sawa na upungufu wa **asilimia 65.6** ikilinganishwa na mwaka 2023/2024; na

(iii) Kwa ujumla, kuna mwenendo wa kupanda kisha kushuka, na kupungua kwa jumla ya **asilimia 43.6** kati ya mwaka 2022/2023 na 2024/2025.


Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mwenendo wa riba na marejesho ya mikopo unaonyesha kupanda kwa kasi mwaka 2023/2024 kisha kushuka kwa kasi kubwa mwaka 2024/2025, na kupungua kwa jumla kwa asilimia 43.6 katika kipindi cha miaka mitatu. Kamati ilifuatilia zaidi na kubaini kushuka huku kwa mwaka 2024/2025 kulitokana na Mamlaka ya Bandari kumaliza mkopo wake ambapo mapato yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yaliiwezesha mamlaka kulipa deni lake lote.

(e) Makusanyo kutokna na Mfumo wa Ufuatiliaji wa Trafiki ya Mawasiliano (TTMS)

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11(2)(o) kinamwelekeza Msajili wa Hazina kufuatilia Ruzuku za Mitaji, Ruzuku ya Kusaidia Uendeshaji, Fedha za Mtaji kwa Uwekezaji wa Muda Mrefu, Akiba na Mapato Yaliyobaki. Mapato kutokana na Mfumo wa Ufuatiliaji wa Trafiki ya Mawasiliano (TTMS) ni

sehemu ya mapato yasiyo ya kikodi yanayostahili kukusanywa na Msajili wa Hazina. Ili kujiridhisha na ukusanyaji wake, tathmini imefanyika kwa miaka mitatu na mwenendo wake unaonekana katika Grafu Na. 7.

Grafu Na. 7: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato kutokana na TTMS kwa kipindi cha 2022/2023 hadi 2024/2025



Chanzo: *Tathmini ya Ukusanyaji wa Mapato kutokana na TTMS kwa kipindi cha 2022/2023 – 2024/2025*

Mheshmiwa Spika, uchambuzi unabainisha yafuatayo:-

(i) Mapato kutokana na TTMS yameendelea kupungua katika kipindi chote cha miaka mitatu;

(ii) Mapato hayo yalipungua kutoka **TSh bilioni 10.11** mwaka 2022/2023 hadi **TSh bilioni 5.94** mwaka 2023/2024 ikiwa ni kupungua kwa asilimia 41.2;

(iii) Mwaka 2024/2025 mapato yalipungua zaidi hadi kufikia **TSh bilioni 3.08**, sawa na **asimimia 48.2** ikilinganishwa na mwaka 2023/2024; na

(iv) Kwa ujumla, kuna mwenendo wa kupungua kwa **wasilisho la TTMS** kati ya mwaka 2022/2023 na 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo huu wa kushuka kwa kasi kwa wasioisho la TTMS katika kipindi cha miaka mitatu. Kamati ilifuatili na kubaini kuwa upungufu huu umechangiwa na mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano jambo ambalo haliepukiki, kwa sasa watu wanaweza kupiga simu za kimataifa kwa kutumia *apps* mbalimbali ikiwemo whatsapp.

(f) Mchango wa Taasisi zinazotoa huduma

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba matokeo ya uwekezaji wa Mitaji ya Umma haupimwi kwa kuangalia faida na mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali pekee. Kwa taasisi zenye majukumu ya kijamii na utoaji wa huduma, kipimo chetu kikubwa kinapaswa kuwa ufanisi na ubora katika utoaji wa huduma, ufanisi wa matumizi ya rasilimali na matokeo yanayomfikia mwananchi (*operational efficiency*).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna taasisi ambazo hazionekani kuwasilisha mchango mkubwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali lakini mchango wake kwenye kuchagiza Uchumi wa Nchi kwa ujumla ni mkubwa na unawezesha taasisi ambazo ni za kibiashara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na mafanikio makubwa (multiplier effect). Baadhi ya taasisi hizo ni pamoja na TANROADS, TARURA na REA.

Mheshimiwa Spika, Kamati inamaoni kwamba ifanyike thathimini ya kina kwa mashirika haya na kubainisha mchango wake kiuchumi, na mchango huo utambulike kama unavyotambulika mchango wa kifedha.

2.5 Mambo ya Jumla kuhusu Uendeshaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, fasili ya 11(1) (b) ya Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni, 2025 inaipa Kamati jukumu la kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ilibaini mambo mbalimbali ya kiutendaji ambayo ni pamoja na;-

2.5.1 Umuhimu wa Kufungamanisha Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi na Dira ya Taifa ya 2050

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inalenga kuifanya Tanzania kuwa taifa lenye uchumi shindani, jumuishi na unaozalisha fursa, likiongozwa na maendeleo ya watu, tija, ubunifu na matumizi bora ya rasilimali. Mafanikio ya Dira 2050 yatategemea kwa kiasi kikubwa namna taasisi na mashirika ya umma yanavyotumia rasilimali walizopewa na Serikali katika kufikia malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya 2050 taasisi na mashirika ya umma yana majukumua mbalimbali ikiwemo;- Kusimamia na kuendeleza rasilimali za taifa kama ardhi, madini, nishati, maji na miundombinu; Kuwekeza katika sekta za kimkakati zinazochochea ukuaji

wa uchumi; Kuzalisha mapato na gawio kwa Serikali, hivyo kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia huduma za kijamii na maendeleo; Kuchochea uzalishaji, ajira na biashara kupitia uwekezaji na shughuli za kibiashara; Kuvutia mitaji na teknolojia kupitia ubia na sekta binafsi; na Kutoa huduma muhimu kwa wananchi kwa ufanisi na kwa viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambae ndio msimamizi wa taasisi na mashirika ya umma ameandaa Waraka wa Msajili wa Hazina unaozitaka taasisi zote na mashirika ya umma Kuandaa Mpango Mkakati unaoendana na Mpango wa Maendeleo wa 4 wa Miaka 5 (FYDP4) na Dira 2050. Dhumuni la Waraka huu ni kufungamanisha Mipango mikakati ya taasisi na mipango ya mageuzi iliyomo ndani ya mipango hiyo mikuu ya nchi. Kamati ilifuatilia utekelezaji na kubaini kuwa kuna mwitikio wa utekelezaji wa agizo hili ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, nia njema ya waraka huu ilikuwa ni kuhakikisha taasisi na mashirika ya umma zinahuwisha mipango yake na kuhakikisha malengo yaliyomo katika mikakati mikuu ya nchi yanaakisiwa katika shughuli za kila siku za taasisi na mashirika ya umma. Ni maoni ya Kamati kuwa Msajili wa Hazina asimamie jukumu hili kikamilifu na kuhakikisha taasisi zote za umma ambao ndio wanategemewa kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Nne wa miaka Mitano (5) FYDP4 na

Dira 2050 zinatekeleza kikamilifu waraka huu ili kufanikisha mageuzi yaliyomo katika mipango hii mikubwa ya nchi kwa lengo la kuleta ustawi wa wananchi.

2.5.2 Mpango wa Kushirikisha Sekta binafsi (PPP) katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa na taasisi/mashirika ya umma

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2026/2027 unaiona sekta binafsi kama mshirika wa maendeleo, Mpango huu unalenga kuhama kutoka kutegemea zaidi bajeti ya umma na mikopo kwenda kwenye mfumo wa ugharamiaji shirikishi, unaolenga ushiriki mkubwa wa sekta binafsi. Mpango umeweka lengo la zaidi ya asilimia 70 ya jumla ya rasilimali za Mpango kuhusishwa na sekta binafsi. Ushiriki wa sekta binafsi unatarajiwa katika uwekezaji, miradi ya maendeleo, uzalishaji, ajira, utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha mpango huu unafanikiwa Mashirika ya umma yana nafasi muhimu katika kuifanya sekta binafsi kuwa mshirika wa Serikali katika uwekezaji, uzalishaji, utoaji wa huduma na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Kamati ilikutana na Mradi ambao umetumia PPP na kufanikiwa ambao ni Mradi wa Mabasi yaendayo haraka (BRT) ambapo DART imejenga miundombinu na kisha wakatafuta wawekezaji waendeshaji ambapo kwa sasa wapo wawili UDART na MOFAT.

Kwa kuzingatia mfano huu na manufaa yaliyopatikana katika mradi huu, Kamati imekuwa ikiweka msisistizo kwa taasisi na mashirika ambayo yameonekea na kuwa na fursa ya kushirikisha Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uwekezaji. Baadhi ya taasisi ambazo zilifika mbele ya Kamati na kubainika kuwa na fursa ya kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi yake ni pamoaja na Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO), Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), kampuni ya Mbolea TFC.

Kampuni ya Meli Tanzania (*TASHICO*), ina jukumu mahususi la kujenga meli mpya na kufanya ukarabati wa meli, kwa kipindi kilicholiripotiwa na taarifa hii Kampuni ina uhitaji takribani shilingi trilioni 1.19 ili kufanikisha jukumu hili. Kiasi hiki ni kikubwa na kwa kutegemea fedha kutoka Serikalini miradi hii itachukua muda mrefu mpaka kukamilika kwake.

Kwa upande wa Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* Kamati iliona kuna umuhimu wa kutumia sekta binafsi kwa lengo la kupata mtaji lakini pia kupata ujuzi na teknolojia kutoka kwa wabia ambao wana uzoefu wa kutosha katika sekta ya uvuvi wa Samaki.

Eneo jingine ni Kampuni ya Mbolea Tanzania (*TFC*) ambayo ina jukumu la kuzalisha, kuhifadhi na kusambaza aina zote za mbolea nchini na nje ya nchi. Kwa sasa TFC haizalishi mbolea bali inanunua mbolea kutoka kwa kampuni nyingine. Kamati ilifuatilwa na kubaini kuwa Kampuni inatekeleza mradi wa kusimika kiwanda cha Kuchanganya

Mbolea (Fertilizer Blending Facility), kwa mujibu wa uchambuzi mradi huu umechelewa kukamilika kwa sababu ya changamoto ya upatikanaji wa fedha za utekelezaji ambapo inahitajika takribani shilingi **bilioni 5.6** ili kuukamilisha. Kwa kuendelea kutegemea Ruzuku mradi huu utachukua muda mrefu mpaka kukamilika kwake, adiha, ujenzi wa viwanda vya uzalishaji kama sheria inavyoelekeza ndio utachukua muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Serikali ina maeneo mengi ya kuyahudumia hivyo haiwezi kuelekeza rasilimali zote sehemu moja, ni maoni ya Kamati kuwa taasisi zitumie fursa ya kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu yake hususani miradi ya uwekezaji kwa lengo la kufanikisha kwa wakati na kuipunguzia Serikali mzigo.

2.5.3 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini katika Mishahara na uendeshaji

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma kwa lengo la kuhakikisha huduma stahiki zinatolewa ili kuleta ustawi wa jamii na mashirika yanajiendesha kwa tija na faida inapatikana na kuweza kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali lakini pia mashirika yanaweza kujitegemea na kujitoa katika utegemezi wa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya vigezo vya upimaji wa utendaji wa taasisi/shirika ni kuhakikisha utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini unapungua mwaka hadi mwaka.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mashirika yamejitahidi kuzingatia kigezo hiki ambapo kwa mujibu wa taarifa ya utendaji wa Msajili wa Hazina kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 utegemezi wa Ruzuku umepungua kutoka **asilimia 39.1** mwaka 2022/2023 hadi **asilimia 34.2** mwaka 2023/2024 na kisha kufikia asilimia 32 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa licha ya utegemezi kwa ujumla kupungua, lakini bado kuna mashirika ambayo yameweza kuzalisha mapato ya ndani makubwa lakini bado yanapokea ruzuku wanayopokea kutoka Serikali. Aidha, kuna mashirika yanafanya biashara lakini bado yanapokea ruzuku kutoka Serikali hata kwenye kipengele cha mishahara na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kufanikisha azma njema ya kuwa na taasisi na mashirika yenye ufanisi katika utendaji bila kuwa na utegemezi mkubwa wa ruzuku kutoka Serikalini, Msajili wa Hazina ambae ndio msimamizi wa taasisi na mashirika ya uma ana jukumu la kuyawezesha mashirika na kuhakikisha yanatekeleza majukumu yake kikamilifu, yanakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji mapato na yanadhibiti matumizi yake.

Ni rai ya Kamati kuwa, Msajili wa Hazina afanye tathmini na kubaini kiasi halisi cha utegemezi wa Ruzuku ya Serikali, aidha, uandaliwe mkakati wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu wa kuyaondoa mashirika katika utegemezi wa ruzuku kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo.

2.5.4 Tathimini ya Utendaji wa taasisi na Mashirika ya umma

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370, Kifungu cha 7 (1) imempa Msajili wa Hazina jukumu la kusimamia uwekezaji na mali nyingine za Serikali katika taasisi, mashirika, wakala za Serikali na kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa au kuna maslahi ya umma kwa niaba ya Mhe. Rais na kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la ufuatiliaji wa tija ya mitaji katika taasisi na mashirika ya umma, Kamati ilipitia taarifa za utendaji wa baadhi ya taasisi ili kujiridhisha kuhusu utendaji wake. Uchambuzi ulihusisha kuangalia vyanzo vya mapato; mwenendo wa mapato yanayopatikana kama yanatosha kuendesha shughuli mbalimbali za taasisi hizo; matumizi ikilinganishwa na ukomo wa bajeti; ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za taasisi; madeni ya taasisi na mwenendo wa ulipaji; na faida inayopatikana kutokana na utendaji.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kuna baadhi ya Taasisi, Mashirika na Wakala za Serikali utendaji wake unasuasua, jambo ambalo linaathiri tija ya uwekezaji wa mtaji wa umma. Mambo yaliyobainika katika uchambuzi wa Kamati ni pamoja na:-

i) Upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi

Mheshimiwa Spika, taasisi au shirika la umma linapaswa kutekeleza miradi ya uwekezaji ili kutimiza majukumu yake, kuchangia maendeleo ya taifa, kuboresha huduma, kuongeza tija na kulinda au kuongeza thamani ya mtaji wa umma uliowekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wa kiuwekezaji, mradi wa maendeleo hutekelezwa kwa sababu kuna hitaji halisi na matokeo yanayotarajiwa kwa taasisi, Serikali na wananchi. Uchambuzi wa Kamati kwa taasisi zilizofika mbele yake umebaini kuwa licha ya kuwa na uhitaji wa utekelezaji wa miradi mahususi kwa ajili ya manufaa mahususi lakini kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za miradi hiyo jambo ambalo limepekekea miradi husika kutekelezwa kwa muda mrefu na tija ya mradi husika kutopatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini changamoto hii kwa baadhi ya taasisi ikiwemo **TARI, STAMICO, TASHICO, TAFICO, TAA.** Ni maoni ya Kamati kuwa tathimini ya Kina ifanyike wakati wa kupanga miradi ya maendeleo, tathimini hiyo ihusishe upatikanaji wa fedha, wakandarasi mahiri na mikataba bora ya utekelezaji ili tija inayokusudiwa iweze kupatikana kwa wakati.

ii) Changamoto katika Matumizi ya Mfumo wa Manunuzi NEST kwa mashirika yanayojiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10(k) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Na. 10 ya mwaka 2023 Kinaipa Mamlaka ya

Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (*PPRA*) jukumu la kuamua, kuendeleza, kuanzisha, kutunza na kuboresha mifumo ya kiteknolojia inayosaidia ununuzi wa umma. Kupitia kifungu hiki PPRA imeweka mfumo wa NeST ili kufanikisha manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa taarifa za uwekezaji kwa taasisi zilizofika mbele ya Kamati ilibainika kuwa kwa mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara yanakumbana na mkwamo katika kutumia mfumo wa NeST. Taasisi hizo zimeripoti kuwa michakato inayohitajika ili kufanyya manunuzi katika mfumo wa NeST haitoi unafuu(flexibility) kwa mashirika yanayojiendesha kibiashara na kutakiwa kushindana na nguvu ya soko. Taasisi zilitaarifu kukumbana na changamoto hii ni pamoja na STAMICO,

Mheshimiwa Spika, katika kuifanyia kazi changamoto hii kwa lengo la kupata suluhisho, Kamati ilibaini kuwa PPRA inatoa fursa kwa taasisi kuwasilisha maombi kupitia dirisha maalumu kwa kuzingatia mahitaji taasisi husika. Kamati ilibaini pia licha ya kuwepo na fursa hiyo lakini sio taasisi zote zilizokuwa na taarifa hii. Ni maoni ya Kamati kuwa Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na PPRA wazifahamishe taasisi uwepo wa fursa hii na azielekeze taasisi husika kuwasilisha maombi kwa PPRA ya kufunguliwa dirisha maalumu katika NeST litakalorahisisha mchakato wa manunuzi ili kupata ufanisi na tija inayokusudiwa.

iii) Changamoto ya Ukusanyaji wa madeni (receivable)

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kwa taasisi ambazo zimekuwa zikitoa huduma kwa taasisi nyingine za Serikali imekuwa ikikumbana na changamoto ya madeni (receivables) makubwa ambayo yanaathiri mizania ya vitabu vya taasisi. Kamati imebaini kuwa changamoto hii imetokana na taasisi nyingine za Serikali kupata huduma kutoka kwa taasisi na kisha kushindwa/kuchelewa kulipa madai(payables) kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kutafakari jambo hili Kamati ilibaini kuwa changamoto hii ilikuwepo kwa taasisi ya GPSA na TEMESA pia na taasisi hizi ziliamua kuanzisha utaratibu wa malipo kabla ya kupokea huduma, utaratibu huu umesaidia sana kupunguza changamoto ya madeni (receivables) jambo ambalo lina tija kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa taasisi ziimarishe mikakati ya kufuatilia madeni na kuyakusanya kwa lengo la kusafisha mizania ya vitabu vyake. Aidha, taasisi ziangalie uwezekano wa kuweka utaratibu wa kulipa kabla ya huduma kwa lengo la kuepuka malimbikizo ya madai ambayo yanaathiri mizania ya vitabu vya taasisi na mtaji wa umma kwa ujumla.

iv) Changamoto ya upungufu wa mtaji

Mheshimiwa Spika, mtaji kwa taaasisi/shirika la umma huathiri moja kwa moja thamani ya uwekezaji na ufanisi wake. Taasisi yenye mtaji unaotosheleza mahitaji yake inaweza kuongeza uzalishaji, kuongeza mapato na faida, na

hatimaye kuongeza uwezekano wa Serikali kupata gawio au manufaa mengine kutokana na uwekezaji wake.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna baadhi ya taasisi/mashirika ya umma yanajiendesha yakiwa na mtaji mdogo au hasi kabisa jambo linaloathiri utendaji wake na tija ya uwekezaji kwa ujumla. Miongoni mwa taasisi zinazojiendesha yakiwa na upungufu mkubwa wa mtaji au mtaji hasi ni pamoja na TFRA ambayo ina upungufu wa mtaji (Mtaji hasi) wa kiasi cha shilingi bilioni 253.18, ATCL mtaji hasi shilingi bilioni 495.59, Mtaji hasi wa UDART shilingi bilioni 169.44, Kampuni tanzu ya TTCL (T Pesa) mtaji wa shilingi milioni 614.81

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali kwa kupitia Msajili wa Hazina ifanyike thathimini ya kina juu mahitaji halisi ya mtaji na Serikali iwekeza mtaji huo kwa lengo la kuyawezesha taasisi/mashirika kujiendesha kwa ufanisi.

v) Mashirika kupata Hasara/nakisi

Mheshimiwa Spika, katika ufuatiliaji wa taarifa za utendaji mashirika/taasisi, Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya taasisi/mashirika ya umma yameendelea kupata hasara/nakisi kwa takribani miaka mitatu mtawalia. Aidha, kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibitin a Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuna jumla ya mashirika ya umma na taasisi zingine za kibiashara 22 zimeendelea kupata hasara kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja hadi mitatu mtawalia.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 8(1)(2) cha Sheria ya Mashirika ya Umma, SURA ya 257, kinataka mashirika ya umma kujiendesha kwa misingi imara ya kibiashara kwa kupata faida halisi ya mtaji uliowekwa ya angalau asilimia 5. Baadhi ya taasisi/mashirika zilizofika mbele ya Kamati na kubainika kuwa yanapata hasara/nakisi ni pamoja na UDART, TTCL Pesa, TFRA, ATCL, CPB n.k.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa mipango ya nchi hutekelezwa na taasisi na mashirika ya umma, inapoonekana kuna mapungufu katika utendaji wa taasisi na mashirika ya umma inaleta mashaka juu ya ukamilivu wa mipango mzuri iliyowekwa na Serikali. Ni rai ya Kamati kwa Bodi za Wakurugenzi wa Taasisi na Mashirika ya Umma kuhakikisha majukumu iliyokasimiwa yanatekelezwa kwa ufanisi na tija iliyokusudiwa iweze kupatikana.

2.5.5 Mapungufu katika Utendaji wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ni taasisi iliyoanzishwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria ikiwa na jukumu kuu la kufanya biashara ya mazao mbalimbali ya chakula na kuweza kutengeneza faida. Ili kufikia lengo hilo, Bodi inatakiwa kuimarisha utendaji wake na kuhakikisha inatekeleza mipango yenye tija na kwa ufanisi mkubwa. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini

mambo mbalimbali ambayo yamekuwa yakiathiri utendaji wa Bodi hii ambayo ni pamoja na :-

Mwenendo wa Hasara: Bodi imekuwa na mwenendo usioridhisha uliopelekea kutengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mtawalia kuanzia mwaka 2022/2023 hadi mwaka 2024/2025 ambapo hasara ilitoka Shilingi bilioni 4.97 hadi kufikia Shilingi bilioni 11.17 ambayo ni ongezeko la hasara kwa asilimia 124.7 na imepelekea kuathiri mtaji wa umma uliowekezwa ambao umeshuka kwa asilimia 48 kwa kipindi cha miaka mitatu.

Utaratibu wa Matumizi ya Mikopo ya Muda Mfupi (*Overdraft Facility*): kama ilivyo kwa taasisi nyingine za kibiashara, Bodi inayo fursa ya kutumia mikopo ikiwa ni miongoni chanzo cha kupata mtaji kwa lengo la kuongeza uwezo wa kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Bodi ilifanya maamuzi ya kutumia mkopo wa *overdraft* (*overdraft facility*), aina hii ya mkopo imepelekea kuongezeka kwa mzigo wa madeni na kuathiri mtaji wa Bodi pamoja na kushusha ufanisi wa kimajukumu kutokana kwa kuwa masharti ya mkopo huu hayaendani na asili ya biashara inayofanywa na Bodi ambayo ni ya msimu.

Utaratibu wa Ajira za Muda Mfupi: Kamati ilibaini pia uwepo wa changamoto ya utaratibu wa ajira za mikataba ya watumishi yenye ukomo wa miaka miwili. Hali hiyo inaathiri ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za bodi zikiwemo uendeshaji wa viwanda kwani hutumia rasilimali nyingi katika

kuwajengea uwezo na uzoefu watumishi na baada ya muda huondoka mara baada ya kupata fursa za ajira za uhakika na za kudumu mahala pengine, jambo hili linashusha ufanisi na tija ya mtaji uliowekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa Kamati na kwa muktadha wa kuisaidia Bodi ya Mazao Mchanganyiko kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija iliyokusudiwa iweze mkupatikana, ni rai ya Kamati kuwa tathimini ya kina ifanyike kwa lengo la kuangalia namna bora ya kufanya mageuzi ya kiutendaji kwa bodi hii.

2.5.6 Athari ya Deni la Tozo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Kampuni ya STAMIGOLD

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2019 Kampuni ya STAMIGOLD ilielekezwa kuuza dhahabu yake katika soko la ndani pekee ikiwa ni juhudi za Serikali katika kuongeza matokeo ya ukusanyaji wa dhahabu, kuimarisha akiba ya nchi na kuendelea kusimamia ukuaji wa uchumi. Aidha, kabla ya mwaka 2019, Kampuni ilikuwa ikitekeleza shughuli zake za biashara ya dhahabu katika masoko yote ndani na nje ya nchi na ilikuwa kwenye msawazo (fair ground) ya ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati imebaini kuwa wakati maelekezo yanatolewa kwa STAMIGOLD hayakuwekewa mwongozo mahsusi ili kuhakikisha Kampuni inaendelea kujiendesha kwa ufanisi na kiushindani. Kukosekana kwa mwongozi pia kulipelekea mkanganyiko baina Kampuni na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambapo mwishoni mwaka 2025 TRA ilifanya mapitio ya

mwenendo wa biashara ya STAMIGOLD na hali ya ulipaji wa kodi (VAT) ya Kampuni na kubaini uwepo wa limbikizo la deni la takribani Shilingi 26,075,583,464 na riba ya Shilingi 5,774,693,283 inayofanya jumla ya Shilingi 31,850,276,747 kwa kipindi cha miaka sita (6) kuanzia mwaka 2019 hadi 2024.

Mheshimiwa Spika, Sheria umeweka unafuu wa kutotoza kodi ya VAT kwa kampuni inayouza bidhaa yake nje huku kampuni inayouza ndani kulazimika kulipa kodi hiyo. Hivyo basi kwa STAMIGOLD kutekeleza maelekezo hayo mhususi bila ya kuwepo na mwongozo thabiti kumeiweka Kampuni katika hali ya kuathirika kimtaji na kiushindani.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kwamba, Kwakua Serikali ilitoa agizo ili kuweza kunufaika kimakusanyo na akiba jambo ambalo limekuwa na mafanikio makubwa, hivyo basi Wizara ya Fedha kupitia TRA itathimini na deni la VAT lililozalishwa wakati wa utekelezezaji wa agizo liondolewe katika vitabu vya Kampuni ili kuimarisha mtaji wa Kampuni. Vile vile, Serikali iiwekee STAMIGOLD utaratibu ambao utaendelea kuisaidia Serikali kuimarisha makusanyo na akiba huku ukiifanya Kampuni kuendelea kukuza mtaji na kumudu ushindani wa kibiashara.

2.5.7 Changamoto ya Madeni kwa Mamlaka ya Mbolea (TFRA)

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya mbolea Tanzania (TFRA) pamoja na majukumu yake ya msingi (udhibiti) imeongezewa jukumu la kusimamia ruzuku ya Mbolea nchini. Kwa lengo la kutekeleza jukumu hilo Serikali imekuwa

ikitenga bajeti ya Ruzuku ya Mbolea ambapo kwa mwaka 2022/2023 ilitenga shilingi bilioni 150, mwaka 2023/2024 shilingi bilioni 150 na mwaka 2024/2025 ilitenga shilini bilioni 230.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia mtaji wa umma unaotumika katika mamlaka hii, Kamati imebaini kuwa kumekuwa na tofauti ya bajeti inayotengwa na fedha zinazopokelewa. Aidha, Kamati imebaini pia, kumekuwa na tofauti kubwa kati ya fedha za ruzuku zinazotolewa na kiasi kinachotumika kila mwaka jambo linalosababisha nakisi katika vitabu vya TFRA. Nakisi hii ni fedha ambazo wafanyabiashara waliosambaza mbolea wanaidai Serikali.

Mheshmiwa Spika, Kwa mujibu wa hesabu za TFRA zilizokaguliwa na CAG katika kipindi cha mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025 zinaonesha kuwa madeni ya Mamlaka yameongezeka na kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 264.16. Hali hii ya madeni imeathiri mtaji wa TFRA hadi kufikia kuwa na mtaji hasi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya mtaji imepelekea kuzalisha madeni makubwa ambayo yamepelekea kuathiri ufanisi wa mamlaka. Ni rai ya Kamati kuwa kwa kuzingatia umuhimu wa jukumu linalotekelezwa na mamlaka, Serikali itafute mpango wa haraka wa kuiwezesha kulipa madeni yake na bajeti ya ruzuku itengwe kulingana na makadirio halisi ya mahitaji ili kuepuka madai mapya yasiyoweza kutengewa fedha.

2.5.8 Mwenendo wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) ni taasisi iliyoanzishwa chini ya Sheria Na.08 ya mwaka 2024 inayoipa majukumu ya kuanzisha, kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege vya Serikali katika eneo la Tanzania Bara. Utekelezaji wa majukumu hayo hutegemea uthabiti wa Mamlaka katika kusimamia ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi, upangaji wa mipango unaozingatia ongezeko la mahitaji na uimara katika kutekeleza miradi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini uwepo wa mapungufu mbalimbali yanayoathiri mwenendo wa Mamlaka katika kufikia tija ya uwekezaji inayokusudiwa ikiwa ni pamoja na uwiano usioridhisha kati ya makusanyo na matumizi ambapo kasi ya ukuaji wa matumizi iko juu ukilinganisha na kasi ya ukuaji wa mapato. Aidha, Mamlaka haina mipango endelevu inayoakisi ukuaji wa maeneo ya kimkakati ikiwemo Dar es Salaam na sekta za kiuchumi kiujumla.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine lililobainika ni kuwa Mamlaka ina miradi mingi ambayo utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua. Mfano, mradi wa usimikaji wa Mifumo ya TEHAMA katika kiwanja cha ndege Songea ulioanza Aprili, 2024 na ulitarajiwa kukamilika Julai, 2025 umefikia asilimia 5 pekee; Mradi wa usanifu wa kina wa kiwanja cha ndege Njombe kwenda Daraja la 4E ulioanza

Januari, 2024 na ulipangwa kukamilika Januari, 2026 kwasasa umefikia asilimia 60; Mradi wa usimikaji wa taa za kuongozea ndege (AGL) kiwanja cha ndege Arusha ambao ulianza Januari, 2024 na ulikusudiwa ukamilike Januari, 2026 umefikia asilimia 25: Mradi wa uondoaji wa mabaki ya tairi kwenye barabara ya kuruka na kutua ndege JNIA ulioanza Januari, 2024 na ulipangwa ukamilike Oktoba, 2024 ambao umefikia asilimia 73: Mradi wa ukamilishaji wa ujenzi wa Jengo la abiria kiwanja cha ndege Mwanza ulioanza Aprili, 2024 na ulipangwa kumalizika Oktoba, 2025 kwasasa umefikia asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi katika eneo la miradi umeonesha kuwa jumla ya miradi ya uwekezaji 46 ilianzishwa ili kutekelezwa na Mamlaka katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Agosti, 2027. Aidha, miradi 18 imekamilika na 28 ikiwa katika hatua mbalimbali. Uchambuzi umeendelea kuonesha kuwa miradi 10 muda wake umeisha licha ya utekelezaaji wake kuwa chini kati ya asilimia 5 na 73.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini Kamati ina maoni kuwa ifanyike tathmini ya kina kwa ajili ya kufanya maboresho na kuimarisha utendaji wa Mamlaka ili iweze kuchangia ipasavyo (*maximum potential*) katika mnyororo wa uchumi na kutoa tija inayotakiwa.

2.5.9 Athari za Upungufu wa Usimamizi wa Rasilimali katika Kampuni ya Ranchi za Taifa (*NARCO*)

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ranchi za Taifa (*National Ranching Company Limited-NARCO*) ilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni (Sura 212), na kupewa majukumu ya kushughulikia ufugaji wa kisasa wa ng'ombe hususani ng'ombe wa nyama kwenye mashamba makubwa ya kibiashara. Aidha, NARCO inaendesha ranchi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa na dhamira ya kuwa kampuni kinara katika uzalishaji wa mifugo kwa viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya NARCO ni taasisi ya kibiashara hivyo inapaswa kuzingatia misingi yote ya kibiashara ikiwemo kupata faida, kutoa gawio kwa Serikali na mtaji kukua kutokana na faida inayopatikana. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hali haiko hivyo ambapo mtaji wa kampuni ulipungua kwa asilimia 4 kutoka shilingi bilioni 151.9 mwaka 2023/2024 hadi kufikia bilioni 145.5 mwaka 2024/2025. Aidha, madeni ya kamapuni yaliongezeka kwa asilimia 11 kutoka Shilingi bilioni 20.5 mwaka 2023/24 hadi Shilingi bilioni 22.7 mwaka 2024/2025.

Kamati ilibaini pia NARCO haina taarifa sahihi ya idadi ya Ranchi inazomiliki pamoja na ukubwa wa ranchi hizo, jambo ambalo linaashiria upotevu wa mapato ya Kampuni. Pia ilibainika kuwa kampuni inatoza ada ya kiasi cha shilingi Elfu Tatu na Mia Tano (3,500) kwa ekari kwa mwaka kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na uhalisia na baadhi ya wanaopatiwa maeneo haya hukodisha (sub-letting)

wafugaji na kujipatia kipato zaidi ambacho kwa mtazamo wa Kamati NARCO ndio walipaswa kutoza kiasi hicho.

Vilevile, Kampuni inauhaba wa vitendea kazi, mfano Kampuni inamiliki burdozer moja tu ambalo linapaswa kuhudumia ranchi zote nchini jambo linalosababisha miundombinu ya baadhi ya ranchi kuwa mbovu. Na kuna baadhi ya ranchi hazitumiki kikamilifu hivyo kupelekea kuwa na uvamizi wa maeneo hayo kutoka kwa watumiaji wengine wa ardhi wakiwemo wakulima na wafugaji na kupelekea migogoro.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na NARCO mwezi Agosti 2023 na kutoa maelekezo kuwa Kampuni inaandae mpango mkakati wa kukuza soko la bidhaa zake ili kuongeza mapato kwani hesabu za Kampuni zilionesha kuwa mapato yake yameshuka kwa takribani asilimia 50 hali inayohatarisha uhai wa Kampuni.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Kampuni iliandaa Mpango wa mabadiliko wa Kampuni wenye thamani ya shilingi bilioni 446 ambao unajumuisha miradi mbalimbali ikiwemo uzalishaji wa mifugo. Aidha mpango huu hadi sasa haukufanikiwa kupata fedha kwa ajili ya kutekelezwa. Tathmini iliyofanyika inaonesha kuwa NARCO imeandaa maandiko 2 ya miradi ya unenepeshaji wa shilingi Bilioni 4 ambayo yaliwasilishwa katika benki za Equity na TADB, bado maombi haya yapo kwenye hatua za idhini. Kwa sasa Kampuni imeandaa andiko lingine lenye thamani ya shilingi

bilioni 3 kwa ajili ya mradi wa unenepeshaji wang'ombe na kujenga miundombinu ya mifugo

Mheshimiwa Spika, Kutokana na uchambuzi wa Kamati uliofanyika, ni maoni ya Kamati kuwa ili NARCO iweze kupata rejesho la uwekezaji na tija kwa taifa inahitaji kufanyiwa mabadiliko (reforms) makubwa ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwake kwa kushiriki katika mnyororo wote wa kuongeza thamani ya mifugo kwa kuanza na maneo yenye matokeo makubwa na vilevile kushirikisha sekta binafsi.

2.5.10 Uzingatiaji wa Vigezo vya Utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10(2)(d) cha sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu) Sura 370 kinampa Msajili wa Hazina jukumu la kupanga shabaha za kifedha na vigezo vya utendaji (*"set financial targets and other performance criteria")* zitakazotekelezwa na mashirika ya umma. Aidha, Msajili ana jukumu la kupitia utendaji wa kifedha, kutathmini utendaji wa Bodi na menejimenti, pamoja na kufuatilia na kutathmini utendaji wa mashirika ya umma kwa lengo la kuhakikisha unapatikana ufanisi na manufaa yaliyotarajiwa.

Katika kutekeleza jukumu hili, Msajili wa Hazina huandaa vigezo vinavyolenga kupima utendaji wa kifedha, ufanisi wa matumizi ya mtaji, utendaji wa Bodi na menejimenti na utoaji wa huduma. Baadhi ya vigezo vinavyotolewa ni pamoja na

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa majukumu yake Kamati imekuwa ikiangalia namna taasisi/shirika linavyozingatia vigezo vya utendaji na kubaini kuwa baadhi ya taasisi zimekuwa zikijiendesha nje ya vigezo vya utendaji jambo ambalo limekuwa likiathiri ufanisi wake na hivyo kuathiri mtaji wa umma uliowekezwa kwenye taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, moja ya kigezo ambacho Kamati imebaini kuwa kimekuwa hakipewi umuhimu wa kutosha na taasisi nyingi ni kigezo cha ukuaji wa mapato ya ndani. Kigezo hiki kinaelekeza kuwa, mapato ya taasisi/shirika yanapaswa kuongezeka kwa asilimia kumi na kuendelea kwa mwaka. Baadhi ya Mashirika ambayo mwenendo wa ukuaji wa mapato umekua si wa kuridhisha ni pamoja na Bodi ya Chai Tanzania, Kampuni ya Meli Tanzania, Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro (KLICL), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN). Kushindwa kutekeleza kigezo hicho ipasavyo inapelekea taasisi nyingi kushindwa kujiimarisha kimtaji na hivyo kuwa na mwenendo usioridhisha katika kuchangia chumo kwa Serikali kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kigezo kingine ambacho Kamati imebaini ni uwiano wa Madeni kwa Mali. Kigezo hiki kinataka uwiano wa madeni kwa mali usizidi asilimia 50 jambo ambalo limekuwa haliwekewi msukumo kwa baadhi ya mashirika kwani Kamati imebaini baadhi ya mashirika yakiwa na uwiano unaozidi kiwango elekezi kwa kipindi cha miaka

miwili na kuendelea. Mfano wa mashishirika ni ATCL, TTCL, TSN. Kutofikiwa kwa kigezo hiki kunaathiri Mtaji wa taasisi/shirika na hivyo kupunguza ufanisi katika kutekeza majukumu yake jambo linaloipunguzia Serikali mapato yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile kigezo cha gharama za uendeshaji ambacho kinazitaka taasisi na mashirika ya umma kuhakikisha zinabana matumizi kwa kiwango kisichozidi asilimia 50, 55 au 60 cha mapato yake kutegemea na aina na shughuli za taasisi. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa taasisi nyingi zikiwemo Shirika la Mawasiliano (TTCL), Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO), Benki ya TCB, Kampuni ya Uzalishaji Bidhaa za Ngozi – Kilimanjaro (KLICL), Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO), Benki ya TIB, Shirika la Taifa la Utangazaji (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) n.k. Kushindwa kuzingatiwa kwa kigezo hiki kunaathiri taasisi hizo kukua kimtaji, kukosa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya msingi na kukosekana kwa tija kusudiwa ikiwemo kutofikiwa kwa chumo stahiki (effective divident) na uchangiaji mdogo wa michango mingineyo.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya utendaji huwekwa kama nyenzo inayokusudiwa kuiongoza Bodi za Wakarugenzi na Menejimenti wa Taasisi/shirika la umma katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi yake, Ni maoni ya Kamati kuwa ili kufanikisha dhamira ya uwekezaji wa mtaji katika

taasisi/shirika husika watendaji hawa wakuu wajielekeze kujiendesha ndani ya vigezo walivyopewa kwa lengo la kuleta ufanisi na kupata tija iliyokusudiwa.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni Kutokana na Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imefanya ufuatiliaji wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Serikali kwa niaba ya Bunge lako Tukufu. Katika kutekeleza jukumu hilo taasisi mbalimbali zilifika mbele ya Kamati ambapo pamoja na mambo mengie ilijielekeza kuangalia taswira nzima ya ongezeko la thamani ya uwekezaji; tija na ufanisi; gawio na mapato kwa Serikali pale yanapostahili; kupungua kwa utegemezi; utawala bora; pamoja na huduma bora na zenye matokeo kwa wananchi, na pia inatarajiwa kuwa ukuaji wa uwekezaji wa umma uendane pia, na kuleta matokeo yanayoakisi ukuaji huo.

3.1.1 Ongezeko la Mtaji wa Umma

Mtaji wa umma umeongezeka kwa asilimia 20.3, huku rejesho likiongezeka kwa asilimia 2 pekee. Kamati inasisitiza kuimarisha usimamizi ili kuongeza tija na rejesho la uwekezaji.

3.1.2 Uwekezaji katika Taasisi Ambazo Serikali Inamiliki Hisa Chini ya Asilimia 50

Ongezeko la thamani ya uwekezaji katika taasisi Taasisi Ambazo Serikali Inamiliki Hisa chache hadi ongezeko la asilimia 152 ni ishara ya fursa za sekta binafsi kuongeza tija ya mtaji wa umma.

3.1.3 Michango ya Mashirika ya Umma katika Mfuko Mkuu wa Serikali

Kutokuwepo kwa vigezo madhubuti kunasababisha kutokuwiana kwa michango ya mashirika ya umma. Hali hiyo inahiatji kuwekwa kwa viwango vinavyozingatia uwezo wa kifedha na kuimarisha uwajibikaji.

3.1.4 Utegemezi wa Ruzuku ya Serikali

Bkuendelea kuwepo kwa mashirika yenye uwezo wa kujipatia mapato lakini yanategemea ruzuku ya Serikali ni jambo linalohitaji mikakati mahususi ya kuimarisha uwezo wa mashirika kujitegemea kifedha.

3.1.5 Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma

Changamoto za kiutendaji katika baadhi ya mashirika zinahatarisha tija ya mtaji wa umma. Kufanyika kwa tathmini ya kina na kuweka hatua mahsusi za maboresho ni jambo linalohitajika.

3.1.6 Ushirikiano na Sekta Binafsi katika Miradi ya Maendeleo

Changamoto ya kutokutumika kikalifu kwa fursa za sekta binafsi katika kugharimia miradi ya uwekezaji ya mashirika ya umma, kunaweza kutatutiwa kwa kuweka utaratibu wa kuvutia mitaji na kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali.

3.1.7 Madeni ya Ruzuku ya Mbolea kwa TFRA

Kulipa madeni ya ruzuku ya shilingi bilioni 264.16 kwa NFRA ambayo yanaathiri mzunguko wa mtaji wake na

wafanyabiashara ni jambo linalohitaji kufanyika angalau kwa awamu.

3.1.8 Deni la VAT la STAMIGOLD

Deni la VAT la shilingi bilioni 31.85 linalongeza mzigo wa kifedha kwa STAMIGOLD linastahili kushuighulikiwa kwa mujibu wa sheria ili kuimarisha uwezo wa Kampuni kuwekeza.

3.1.9 Mipango ya Taasisi na Dira ya Taifa ya 2050

Mipango mikakati ya baadhi ya taasisi kutofungamanishwa na Mpango wa nne wa wa Taifa wa Miaka mitano ni jambo linaloweza kuathiri tija ya mtaji wa umma.

3.1.10 Utendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA)

Kuchelewa kwa Miradi 10 kati ya 46 ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kunachelewsha upatikanaji wa manufaa ya uwekezaji. Hivyo, upo umuhimu wa kuimarisha mipango na usimamizi wa miradi ili kuongeza tija ya mtaji wa umma.

3.1.11 Usimamizi wa Rasilimali za NARCO

Upungufu katika usimamizi wa ranchi na tozo za ukodishaji unapunguza tija ya mtaji wa umma. Uhakiki wa rasilimali, kuboresha matumizi yake na kupitia tozo za ukodishaji ni mambo muhimu yanayoweza kuongeza tija ya mtaji wa umma uliowekezwa katika NARCO .

3.1.12 Uzingatiaji wa Vigezo vya Utendaji

Baadhi ya taasisi na mashirika ya umma kutozizingatia vigezo vya utendaji vya Msajili wa Hazina, ni jambo linalohatarisha

tija ya mtaji wa umma. Hivyo, kuimarisha ufuatiliaji na uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti ni suala linalostahili kupewa kipaumbele.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchambuzi uliofanywa na Kamati, naomba kubainisha mapendekezo ya Kamati ambayo kwa mtazamo wa Kamati, iwapo Bunge litaridhia yanakusudia kutatua changamoto zilizopo katika uwekezaji wa mitaji ya Umma na hatimaye kuongeza ufanisi wa Uwekezaji mkubwa uliofanya na unaoendelea kufanywa na Serikali.

3.2.1 Ongezeko la Mtaji wa umma katika taasisi na Mashirika ya Umma

KWA KUWA, Mtaji wa Umma katika taasisi na mashirika ya umma umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka hadi kufikia shilingi trilioni 92.275, sawa na ongezeko la asilimia 20.3 kwa kipindi cha miaka mitatu;

NA KWA KUWA, katika kipindi cha miaka mitatu, rejesho kwa mtaji wa umma limeongezeka kwa asilimia 2 ilhali uwekezaji umeongezeka kwa asilimia 20.3, hali inayoibua hoja kuhusu ufanisi wa mtaji wa umma na manufaa yake kwa wananchi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, -

(i) Serikali kupitia Msajili wa Hazina iimarishe usimamizi na ufuatiliaji wa mtaji wa umma katika mashirika ya umma; na

(ii) Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe kuwa ongezeko la thamani ya uwekezaji linawiana na ongezeko la rejesho katika muundo wa uzalishaji, mapato na manufaa kwa wananchi.

3.2.2 Ongezeko la Thamani ya Uwekezaji katika taasisi ambapo Mtaji wa umma ni pungufu ya asilimia 50

KWA KUWA, Thamani ya uwekezaji mtaji wa umma katika taasisi ambapo Serikali inamiliki hisa chini ya asilimia 50 imeongezeka kwa asilimia 152 katika kipindi cha miaka mitatu,

NA KWA KUWA, Ongezeko hilo linaashiria uwezekano wa kupata manufaa makubwa ya mtaji wa umma kupitia ushirikiano na sekta binafsi ili kuongeza tija na faida ya uwekezaji huo,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kubaini na kutumia fursa za uwekezaji katika mashirika ambayo inamiliki hisa asilimia 50 au chini yake, kwa lengo la kuongeza faida na manufaa yatokanayo na uwekezaji wa mtaji wa umma.

3.2.3 Mchango wa Mashirika ya Umma katika Mfuko Mkuu wa Serikali

KWA KUWA, pamoja na kuwepo kwa matakwa ya kisheria kuhusu uchangiaji wa taasisi na mashirika ya umma katika Mfuko Mkuu wa Serikali, utekelezaji wake hauna utaratibu madhubuti unaoainisha viwango vya michango na uwajibikaji wa taasisi zinazohusika;

NA KWA KUWA, hali hiyo inachangia kutokuwiana kwa viwango vya michango kati ya taasisi na mashirika ya umma na kuibua changamoto ya uhakika kwa kila taasisi kutekeleza wajibu huo kwa kuzingatia uwezo wake na matakwa ya kisheria;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, ichukue hatua zifuatazo:

(i) Kuhakikisha kuwa kila taasisi na shirika la umma linachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria;

(ii) Kuchambua taasisi na mashirika ya umma na kuainisha vigezo na viwango vya michango kwa kuzingatia majukumu, hali ya kifedha na uwezo wa kila taasisi au shirika, utekelezaji wa masharti ya Sheria uendane na uhalisia; na

(iii) Kuweka utaratibu madhubuti wa kufuatilia na kuwawajibisha Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za taasisi na mashirika ya umma zinazoshindwa kutekeleza

wajibu wa kisheria wa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

3.2.4 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini

KWA KUWA, baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yana uwezo wa kuwa mapato ya ndani toshelevu, lakini bado yanaendelea kutegemea ruzuku ya Serikali kugharimia mishahara na shughuli za uendeshaji;

NA KWA KUWA, hali hiyo inaonesha kuwepo kwa changamoto katika uwiano kati ya uwezo wa taasisi kujipatia mapato na mipango ya kupunguza utegemezi wa ruzuku, jambo linaloweza kudhoofisha juhudi za kujitegemea kifedha na kuathiri ufanisi wa rasilimali za umma katika uwekezaji,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, iimarishe mikakati ya kupunguza utegemezi wa ruzuku kwa taasisi na mashirika ya umma kwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kufanya tathmini ya taasisi na mashirika ya umma ili kubaini kiwango cha utegemezi wa ruzuku ya Serikali na uwezo wake wa kujitegemea kifedha;

(ii) Kuweka mikakati ya muda wa kati, isiyozidi miaka mitatu, kwa taasisi na mashirika ya umma yanayofanya biashara ili kupunguza na hatimaye kuondokana na utegemezi wa ruzuku ya Serikali;

(iii) Kuweka mikakati ya muda mfupi kwa taasisi na mashirika ya umma ambayo mapato yake ya ndani yanazidi kiasi cha ruzuku inayopokea, ili yaondokane na utegemezi huo; na

